JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
KURUGENZI YA MAWASILIANO YA RAIS, IKULU

***Dar es Salaam***
***05 Juni, 2025***

**TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI**

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan ametoa wito kwa jamii kushirikiana kuwatunza, kuwawezesha na kuwajali watoto wenye mahitaji maalum.

Akizungumza wakati wa kilele cha harambee ya kuchangia ujenzi wa Kituo cha Kulelea Watoto wenye Mahitaji Maalum cha Bagamoyo *(Bagamoyo Diaconic Lutheran Centre),* iliyoandaliwa na Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) katika Ukumbi wa Diamond Jubilee, Rais Dkt. Samia amesema kuwa watoto wenye ulemavu hawapaswi kufichwa wala kutengwa, bali wapewe fursa sawa ya malezi, elimu na ustawi kama watoto wengine.

Vilevile, Rais Dkt. Samia amesisitiza dhamira ya Serikali kuendelea kushirikiana na wadau wa maendeleo, wakiwemo viongozi wa dini, mashirika yasiyo ya kiserikali, wadau wa sekta binafsi na wabia wa kimataifa katika kuhakikisha upatikanaji wa huduma bora kwa watoto wenye mahitaji maalum.

Rais Dkt. Samia pia amesisitiza umuhimu wa kudumisha mtazamo chanya kuhusu watoto wenye changamoto mbalimbali za kiafya na kwa jamii kuachana na imani potofu zinazochangia watoto hao kufichwa au kutengwa, na badala yake amewahimiza Watanzania kuendeleza moyo wa upendo na mshikamano kwa kushiriki katika shughuli zinazolenga kusaidia makundi yenye mahitaji maalum katika jamii.

Kadhalika, Rais Dkt. Samia ameeleza kuwa Serikali imekuwa ikichukua hatua madhubuti katika kuimarisha mazingira ya malezi na elimu kwa watoto wenye mahitaji maalum, ikiwa ni pamoja na kuandaa walimu na wataalamu wa afya husika, kujenga miundombinu rafiki

mashuleni na kutoa huduma maalum kama tiba kwa vitendo, mazoezi ya viungo, tiba ya matamshi na huduma za kisaikolojia.

Aidha, Dkt. Rais Samia amebainisha kuwa tayari zaidi ya watoto 1,400 wamesajiliwa katika shule maalum 18 nchini, huku Serikali ikiendelea kuimarisha mfumo wa utoaji huduma hizo kwa kushirikiana na taasisi za dini na mashirika binafsi.

Rais Dkt. Samia pia amelipongeza Kanisa la KKKT kwa mchango wake na kazi inalofanya kuwahudumia watoto wenye mahitaji maalum, ikiwemo kwa kuanza ujenzi wa kituo kingine cha kuwahudumia watoto hao, na ameahidi kuwa Serikali itashirikiana na KKKT kukamilisha na kuendesha kituo hicho, huku akitoa rai kwa taasisi nyingine na watu binafsi kuchangia juhudi hizo kwa moyo wa kujitolea.

Kwa upande wake, Mkuu wa Kanisa la KKKT, Askofu Dkt. Alex Gehaz Malasusa amepongeza ushirikiano uliopo baina ya Serikali, sekta binafsi na wananchi katika kujenga jamii jumuishi na amepongeza jitihada za Maafisa Ustawi wa Jamii za kuhamasisha wazazi kutowaficha watoto wenye changamoto mbalimbali za kiafya ikiwemo ulemavu.

Pamoja na hayo, Askofu Dkt. Malasusa pia amemshukuru Rais Dkt. Samia kwa moyo wa upendo na ushirikiano katika kukuza maendeleo ya kimwili na kiroho kwa watoto wote wa kitanzania, na ametoa shukrani kwa Serikali, taasisi mbalimbali na Watanzania walioguswa na kuchangia maendeleo ya ujenzi wa kituo hicho.

Shaaban Kissu
Naibu Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu